# MORUWASA YETU

MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI NA MAZINGIRA MOROGORO | Toleo Maalum | Januari-Disemba, 2023



# MHESHIMIWA AWESO ARIDHISHWA NA KASI YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA MAJI KIHONDA, ASISITIZA 2023 NI ZAMU YA KIHONDA KUNYWA MAJI

# UJUMBE WA MKURUGENZI MTENDAJI

**Ndugu Msomaji,**

Ninapenda kuchukua nafasi hii kukukaribisha kusoma jarida la **MORUWASA YETU** ambalo ni toleo la kwanza na maalum lenye lengo la kuelimisha umma kuhusu shughuli na masuala mbalimbali yanayofanywa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro **(MORUWASA).**

Katika jarida hili pamoja na mambo mengine msomaji ataweza kupata uelewa kuhusu shughuli na matukio mbalimbali na muhimu yaliyojiri ndani ya Mamlaka katika kipindi cha mwaka 2023.

Matukio mbalimbali yanayogaziwa katika jarida hili yanayohusu utekelezaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira hasa katika maeneo ya mashirikiano na ushirikishwaji wa wadau, utoaji wa elimu kwa umma, utekelezaji wa miradi ya maji, Kurudisha kwa Jamii, Mafunzo na kubadilishana uzoefu yameangaziwa katika jarida hili.

Tunapomaliza mwaka wa 2023 na kuanza mwaka mpya wa 2024, ninapenda kutumia fursa hii kuendelea kuwashukuru wateja na wadau wote wa MORUWASA kwa ushirikiano mkubwa waliotuonesha katika kipindi chote cha mwaka 2023.

Aidha kwa upekee tunatoa shukrani za dhati kwa Rais wa Awamu ya 6 Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan na Wizara ya Maji kwa kutuwezesha kwa kutekeleza ahadi ya **2023 Mwaka wa Kihonda** kwa wananchi wa maeneo ya Kihonda, Lukobe, Mkundi na Kiegea kupitia mradi wa kuboresha huduma ya maji katika kata za Kihonda, Lukobe na Mkundi wenye gharama ya takribani shilingi **Bilioni 18.**

Tunaahidi kuendelea kuhabarisha umma kuhusu kazi na shughuli za Mamlaka kupitia jarida la **MORUWASA YETU** katika matoleo yatakayofuata ambayo yatakuwa yanatoka kila baada ya miezi mitatu (Robo ya mwaka wa fedha).

Ninaamini kuwa kupitia Jarida hili wasomaji wetu watapata fursa ya kuelimika na kuwa mabalozi wazuri wa kuelimisha wengine kuhusu shughuli zinazotekelezwa na MORUWASA.

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi Menejimenti na Watumishi wote wa MORUWASA ninawatakia wadau wetu wote kheri ya Mwaka Mpya 2024.



**Mhandisi Tamim T. Katakweba**
**MKURUGENZI MTENDAJI**



# FURAHA YATAWALA BIGWA- MRADI WA MAJI BIGWA WAZINDULIWA RASMI NA MHE. AWESO.

Waziri wa Maji ,Mhe.Jumaa Aweso alizindua rasmi Mradi wa kuboresha Huduma ya Maji wa Bigwa-Bohmela unaonufaisha taribani ya wakazi 39,424 wa maeneo ya Bigwa Sokoni,Bigwa Kisiwani Makuti,Bigwa Sister,Bigwa Ualimu, Lukuyu, Bigwa Relini, Kilakala,Bohmela, Mwanzo Mgumu, Misongeni,Kingolwira na Kitungwa katika Manispaa ya Morogoro.

Akiongea baada ya kuzindua mradi huo Mhe. Aweso alimpongeza Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) Mhandisi Tamim Katakweba na watendaji wake wote kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuhakikisha mradi huo uliogharimu Shilingi Bilioni 2.4 unakamilika kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa na kupelekea kuimarisha huduma ya maji kwa wananchi wa maeneo hayo.

Aidha, Mhe. Aweso aliielekeza MORUWASA na Mamlaka nyingine za Maji nchini kuhakikisha huduma ya maunganisho ya Maji inatolewa kwa wananchi bila vikwazo na pia kuhakikisha zoezi la usomaji wa dira za maji unafanyika kwa ufanisi na kwa kuwashirikisha wananchi.

Hafla ya uzinduzi wa Mradi huo wa maji uliotekelezwa na MORUWASA ulifanyika mapema Januari 04,2023 katika uwanja wa highland -Bigwa na kuhudhuriwa na wananchi na viongozi mbalimbali wa Manispaa ya Morogoro wakiwemo Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro, Dkt. Mussa A.Mussa, Mbunge wa Morogoro Mjini,Mhe. Abdulazizi Abood, Mwenyekiti wa Chama cha CCM Mkoa wa Morogoro, Bw. Fikiri Juma na Diwani wa Kata ya Kilakala, Mhe. Michael Kanga pamoja na Taasisi za Bonde la Wami-Ruvu na RUWASA.



# MHESHIMIWA AWESO ARIDHISHWA NA KASI YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA MAJI KIHONDA, ASISITIZA 2023 NI ZAMU YA KIHONDA KUNYWA MAJI

Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso alifanya ziara ya kukagua ujenzi wa Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji maeneo ya Kihonda,Mkundi,Lukobe,Kiegea,Kilimanjaro,SGR,Viwandani na Yespa ambayo kwa muda mrefu yamekuwa yakikabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa uhakika wa huduma ya maji.

Ziara hiyo iliyofanyika mapema Januari 4, 2023 ilihusisha Ukaguzi wa ujenzi wa mradi wa kituo kipya cha Kusukuma maji (Pump House) eneo la Mizani ambao upo katika hatua za mwisho za utekelezaji na Ujenzi wa Tanki la Maji lenye ujazo wa lita Milioni Moja lililopo eneo la Mlima Magereza,Kiegea pamoja pamoja na ulazaji wa bomba za maji kutoka tanki la Maji la Mgulu wa ndege kuelekea maeneo ya Kihonda Kaskazini, Lukobe na Makunganya.

Akiongea wakati wa ziara hiyo, Mhe. Aweso alimpongeza Mkurugenzi Mtendaji wa MORUWASA, Mhandisi Tamim Katakweba kwa kazi iliyokwishakufanyika katika mradi huu na na kumtaka aongeze nguvu kazi ili kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati na wananchi wa maeneo nufaika wanapata huduma ya maji ndani ya mwaka huu wa 2023.



Mradi huu ambao unagharimu takribani shilingi Bilioni 18 utanufaisha jumla ya wananchi wapatao 120,000 wa maeneo hayo.

## KAMATI YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA YATEMBELEA BWAWA LA MINDU.

Kamati ya kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira imeanza ziara yake ya siku tatu katika Mkoa wa Morogoro leo Oktoba 12, 2023 ambapo pamoja na mambo mengine imeweza kujionea hali ya Bwawa la Mindu na jitihada mbalimbali za uhifadhi wa Bwawa hilo.

Kamati hiyo imeagiza Mamlaka na Taasisi za Serikali kushirikiana katika utoaji wa elimu na ushirikishwaji wa wananchi katika utunzaji wa vyanzo vya maji hususani katika vyanzo vya moto inayotiririsha maji katika Bwawa la Mindu ili kulifanya Bwawa hilo kuwa endelevu.

Kwa upande mwingine Kamati imeshauri juu ya kutumia wataalam wa ndani katika kutekeleza Mradi Mkubwa wa maji katika Manispaa ya Morogoro wenye thamani ya Shilingi Bilioni 185 utakaohusisha unyanyuaji wa tuta Bwawa la Mindu ili kuokoa fedha za Serikali.





# UFUATILIAJI WA MAENDELEO YA MRADI WA KUBORESHA HUDUMA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MOROGORO (AFD).

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji Mha. Mwajuma Waziri aliwataka Wataalam Washauri wa Mradi wa Kuboresha Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (AFD) kuhakikisha wanafanya kazi inayoonekana kwa macho "Site" katika utekelezaji wa Mradi huo.

Alitoa maagizo hayo Novemba 21, 2023 wakati wa kikao cha Ufuatiliaji wa Maendeleo ya Mradi huo wenye thamani ya Tsh. Bilioni 185 na kusisitiza kuwa utekelezaji wa Mradi huo upo nyuma ya muda na hawana budi kuhakikisha wanaongeza kasi.

Katika maagizo yake pia aliwataka Wataalam Washauri wa Mradi huo kukamilisha nyaraka za zabuni ifikapo Disemba 2023.

Pia aliwasisitiza kufanya kazi kwa ushirikiano na kushirikisha wadau ili kuleta tija na matukio mazuri katika utekelezaji wa Mradi huo.

Naye Mkurugenzi Mtendaji, Mha. Tamim Katakweba alisema kuwa watajitahidi kuhakikisha maelekezo ya Naibu Katibu Mkuu yanatekelezwa ili Mradi uweze kukamilika kwa wakati.

Kikao hicho kilienda sambamba na ziara ya kutembelea baadhi ya maeneo yanayohusika katika utekelezaji wa Mradi huo ambayo ni Bwawa la Mindu, eneo la kujenga Mtambo mpya wa kutibu maji Mafiga na Mabwawa ya Kutibu Majitaka Mafisa.





# WANANCHI KIHONDA KUANZA KUNYWA MAJI MAPEMA MRADI UKIENDELEA KUTEKELEZWA.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Mhe. Adam Malima akiambatana na Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa alitembelea na kukagua Mradi wa Kuboresha huduma ya Maji katika Kata za Kihonda, Lukobe na Mkundi ambapo ametembelea Tanki la Maji lenye Ujazo wa lita milioni mbili la Mguru wa Ndege na Kituo cha Kusukuma Maji (Booster Station) kilichopo Mizani Kihonda.

Akiongea wakati wa ziara hiyo Mhe. Malima aliitaka MORUWASA kufanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha sehemu ya wananchi inaanza kupata maji kabla ya Disemba 2023 wakati utekelezaji wa Mradi ukiendelea.

Aidha Mhe. Malima alimshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwakumbuka wananchi wa Morogoro kupitia Mradi huo utakaonufaisha wakazi wapatao 135,000.

Pia alimpongeza Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso kwa ushirikiano wake na kazi kubwa ya kuusukuma Mradi huo kuhakikisha wananchi wa Morogoro wanaondokana na changamoto ya maji.

Sambamba na hilo alizipongeza MORUWASA na RUWASA kwa kazi kubwa na kasi inayoendelea katika kutekeleza Mradi na kuzitaka kuendelea na bidii hiyo hiyo ya kumtua mama ndoo kichwani.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa MORUWASA , Mha. Tamim Katakweba aliahidi kutekeleza Kazi kwa kasi zaidi ili kuanza kuhudumia sehemu ya Wananchi wakati shughuli za kutekeleza Mradi zikiendelea.

Kwa upande mwingine Mhe. Malima aliwataka wananchi wa Morogoro kuiona, kuithamini na kuiunga mkono kazi kubwa inayoendelea kufanywa na Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kutatua changamoto ya maji.



# KATIBU TAWALA AIPONGEZA MORUWASA

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) imepongezwa kwa kazi nzuri inayoifanya katika kuhakikisha huduma ya Mtandao wa uondoshaji majitaka inazidi kupanuka.

Pongezi hizo zimetolewa Oktoba 2 , 2023 na Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro Mhe. Dkt. Mussa Ali Mussa wakati wa kikao cha kujadili Uimarishaji wa Shughuli ya Usimamizi wa Usafi wa Mazingira ndani ya Mkoa wa Morogoro kilichofanyika katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Morogoro.

Mbali na hilo pia amezitaka Taasisi zinazosimamia Usafi wa Mazingira kufuata sheria za nchi na kushirikisha jamii kwa ukaribu juu ya masuala ya kisheria ili kuongeza wigo wa usafi wa Mkoa wa Morogoro.

Kwa upande wake Meneja wa Mazingira na Usafi wa Mazingira, Mhandisi. Gidion Chahe alipokuwa akiwasilisha wasilisho kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji amebainisha kuwa MORUWASA imejipanga kuanza mchakato wa kujenga mabwawa ya kutibu Majitaka katika Miji midogo ya Kilosa na Mikumi.

Ameongeza kuwa Mamlaka inakumbwa na changamoto za kuziba kwa mitaro na Chemba kutoka taka ngumu zinazotupwa kwenye Mitandao ya Majitaka.

Kikao hicho kilihudhuriwa Katibu Tawala wa Mkoa, Mkurugenzi Mtendaji wa MORUWASA, Mkurugenzi wa Bodi ya Bonde la Wami/Ruvu, Meneja Mkoa wa TARURA, Meneja Mkoa wa RUWASA, Meneja wa kanda ya Rufiji na Morogoro wa NEMC na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.



## MORUWASA na WATERNET WAWEKA MIKAKATI YA MASHIRIKIANO KWA MWAKA 2023/2024

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) ikiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ilifanya mazungumzo na Shirika la Waternet kupitia Programu ya Waterworx na kuweka mkakati wa mashirikiano baina yao katika kipindi cha mwaka 2023/2024.

Mikakati hiyo imejikita katika maeneo ya Uhifadhi wa vyanzo vya maji hususani kidakio cha Ngerengere kinachotiririsha maji yake katika Bwawa la Mindu.

Pia Mikakati mwingine ni katika eneo la kudhibiti changamoto upotevu wa Maji kwa kuandika kupitia ufungaji wa 'DMA' kwa ajili ya kubaina na kukabiliana na changamoto hiyo.

Aidha elimu ya masuala ya jinsia katika sekta ya Maji ni mkakati mwingine uliowekwa baina ya MORUWASA na Programu ya Waterworx.

Kwa muda mrefu MORUWASA na Waternet wamekuwa na mashirikiano endelevu katika kuhifadhi vyanzo vya maji na kuboresha huduma ya maji Morogoro.

# WATUMISHI MORUWASA WAHASWA KUZINGATIA SHERIA ZA UTUMISHI WA UMMA

Watumishi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) wamehaswa kufanya kazi kwa bidii na kutimiza wajibu bila kukinzana na sheria na miongozo ya Utumishi wa Umma.

Rai hiyo ilitolewa Novemba 09,2023 na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Umma Jaji Mstaafu Mhe. Hamisa Kalombola alipozungumza na watumishi wa MORUWASA wakati wa ziara ya kikazi ya Tume hiyo ya kutembelea Makao makuu ya MORUWASA.

Mhe. Hamisa alisema kuwa Serikali inajitahidi kuboresha mazingira ya kazi kwenye Taasisi kwani Taasisi zote Umma nchini zinatawaliwa na sheria moja ya Utumishi wa Umma ili kuona haki inatendeka.

Aliongeza kuwa lugha nzuri kwa wananchi ni silaha ya maendeleo ya Taasisi na lengo kuu la mtumishi ni kumtumikia mwananchi.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) Mha. Tamim Katakweba alisema kuwa katika misingi ya kusimamia Utumishi wa umma haki inabaki kuwa haki.

Aidha aliongeza kuwa vyombo vya kusimamia haki za watumishi vimewekwa kwa kufuata ngazi ili kuhakikisha ustawi katika umma unakuwepo.

Mha. Katakweba pia aliishukuru Tume hiyo kwa kutoa elimu kuhusu haki na wajibu wa Mtumishi wa Umma pamoja na kazi na majukumu ya Tume hiyo kwa watumishi wa MORUWASA.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili MORUWASA Bi. Christina Mudogo aliishukuru Tume hiyo kwa kuitembelea na Kuzungumza na Watumishi wa Mamlaka na



# MORUWASA YAMTAKA MKANDARASI KUKAMILISHA MRADI WA MKAMBARANI KWA WAKATI

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) Mha. Tamim T. Katakweba alimtaka Mkandarasi PNR Services Ltd anayetekeleza Mradi wa Maji Mkambarani kuhakikisha anakamilisha Mradi huo kwa wakati ili wananchi waweze kuanza kunufaika na huduma ya maji.

Mha. Katakweba alitoa maagizo hayo tarehe 15.11.2023 wakati wa kikao kazi baina ya MORUWASA, RUWASA na Mkandarasi huyo kilicholenga kujadili Maendeleo ya Mradi huo utakaonufaisha wananchi takribani 24,098 wa vijiji vya Mkambarani, Mkono wa Mara na Pangawe ambapo kwa sasa utekelezaji wake umefikia asilimia 29%.

Mha. Tamim alimuelekeza Mkandarasi kuwa kwa sasa anatakiwa kujikita na kazi ya ujenzi wa bomba kuu la mserereko ( gravity main) lenye kipenyo cha milimita 250 na urefu wa takribani kilomita 6.5 kutoka banio la maji la Bamba hadi kwenye birika la maji lililopo Mlima Ng'aro lenye ujazo wa lita 500,000.

Kwa upande wake Meneja Mradi kutoka PNR Services Ltd Mha. Brahma Reddy alisema kuwa wamepokea maelekezo hayo na kuahidi kuyatekeleza kwa wakati.




## WASILISHO LA MBINU ZA KISASA KUDHIBITI NRW




Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) Bw. Lyang'onjo B. Kiguhe alisema kuwa suala la kupunguza upotevu wa maji ni suala mtambuka kwa watumishi wote hivyo kila mtumishi anawajibu wa kuhakikisha anashiriki katika kupunguza upotevu wa maji yasiyolipiwa.

Aliyasema hayo tarehe 3.11.2023 wakati wa kikao cha wasilisho la mbinu za kisasa za utambuzi wa mivujo lililofanywa na Taasisi ya NEXIS AFRICA LTD katika ofisi za MORUWASA Makao Makuu.

Kwa upande wake Dkt. Joseph Mtamba ambae ni mwakilishi kutoka taasisi ya NEXIS AFRICA LTD alisema kuwa Mamlaka inapaswa kuhakikisha inatumia njia za kisasa katika utambuzi wa mivujo ili kuokoa maji yanayopotea ambayo yanasababisha mapato ya Mamlaka kushuka.

# SEKTYA MAJI TANZANIA YAIBUKA KINARA DUNIANI UTEKELEZAJI MIRADI YA MAJI VIJIJINI

Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika Dkt. Victoria Kwakwa aliitaja na ameipongeza Tanzania kuwa kinara na mfano katika utekelezaji wa programu ya uendelevu wa huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini Mashariki na Kusini mwa Afrika na Duniani kwa kutumumia utaratibu wa malipo kwa matokeo yaani Programme for Results (PforR) ambayo inatekelezwa katika nchi zaidi ya 50 na kufadhiliwa na Benki ya Dunia.

Akizungumza na Waziri wa Fedha Mhe. Dkt Mwigulu Nchemba pamoja na Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso, Makamu wa Rais Kwakwa alisema Tanzania ni mfano bora katika utekelezaji wa Programu ya PforR na ameiomba itoe uzoefu wa mafanikio yake kwa nchi zaidi ya 23 kutoka kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika zinazoshiriki mkutano wa maji na usafi wa mazingira (WASH Leadership Summit).

Awali Tanzania ilipata Dola za Kimarekani milioni 350 katika miaka mitano lakini ndani ya miaka mitatu ya kwanza ilikuwa imefikisha maji kwa zaidi ya watu wapya millioni 4.7 vijijini katika mikoa 17. Kufuatia mafanikio hayo, kulingana na matokeo hayo, Benki ya Dunia imeiongezea Tanzania Dola za Marekani milioni 300 na hivyo kupanua wigo wa utekelezaji kufikia mikoa 25. Kwa sasa shillingi milioni 970 zimepelekwa katika kila Halmashauri kwa ajili ya kuanza utekelezaji.

Aidha, mafanikio haya yamefungua rasmi milango ya uendelevu wa programu hii ambayo inafikia ukomo Julai 2025. Kufuatia hoja ya Tanzania ya kuwa na PforR Awamu ya Pili, Benki ya Dunia imeonesha utayari wa kuwa na PforR Awamu ya Pili katika kipindi cha 2025-2030..

Wizara ya Maji kupitia programu hii ya lipa kwa matokeo (PforR) imetekeleza zaidi ya miradi ya maji 1,500 ambayo imekamilika na inatoa huduma.






## BODI YA WAKURUGENZI MORUWASA YAZINDULIWA RASMI

Waziri wa Maji, Mhe Jumaa Aweso alizindua Bodi 25 za Mamlaka za Maji nchini ikiwemo MORUWASA na kuzitaka bodi hizo na viongozi wa sekta ya Maji kuhakikisha zinatoka huduma za Maji za uhakika sambamba na kuzingatia utoaji wa taarifa kwa wananchi.

Waziri Aweso aliyasema hayo wakati akifungua kikao cha mafunzo ya siku mbili kwa Wakurugenzi wa bodi na Menejimenti za Mamlaka za maji, Septemba 25,2023 jijini Dar es salaam.

Aidha, aliwasisitiza kushirikiana na kujenga mahusiano mazuri na wadau na sekta zingine ili kuleta tija katika utoaji wa huduma za maji.

Vilevile Mhe. Aweso alisisitiza kuhusu kuwekwa kwa mkakati wa kukabiliana na upotevu wa maji yasiyolipiwa (NRW) kwani haikubaliki suala hilo halipaswi kuzoeleka na kuwa jambo la kawaida.

Pia aliwataka kushughulikia changamoto na kero za watumishi na wateja kwa wakati.

Kikao hicho kilienda sambamba na upandishaji wa madaraja wa Mamlaka mbalimbali za Maji nchini kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa ikiwa ni pamoja na upana wa mtandao na kumudu gharama za uendeshaji

## MTAALAMU MSHAURI WA MRADI WA MAJI MOROGORO ASISITIZWA KUKAMILISHA KAZI YA USANIFU KWA WAKATI

Mkurungezi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) Mha. Tamim Katakweba aliwataka wataalam washauri kutoka kampuni ya Egis Water and Martime ya nchini Ufaransa wakishirikiana na kampuni ya Ice Project Service Ltd ya nchini Tanzania kukamilisha taarifa ya mwisho ya usanifu wa Mradi wa Uboreshaji huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro kwa wakati.

Mha. Katakweba aliyasema hayo Septemba 13, 2023 wakati wa kikao na wataalam washauri hao katika ofisi za MORUWASA, Morogoro Mjini.

Pia alisisitiza wataalamu washauri hao kuzingatia ubora na kuhakikisha hadi kufikia Desemba 2023 kazi ya usanifu wa mradi iwe imekamilika ili kuwezesha upatikanaji wa Mkandarasi wa ujenzi wa mradi na kuanza kazi rasmi ya ujenzi ifikapo mwanzoni mwa mwaka 2024 kutimiza azma ya Serikali ya kuhakikisha huduma ya majisafi maeneo ya mijini inafikia asilimia 95 au zaidi ifikapo 2025.

Aidha Mha.Katakweba aliwaahidi ushirikiano wa dhati katika kila hatua ya utekelezaji wa mradi huo.

Kwa upande wake Meneja Mradi kutoka Kampuni ya Egis Water and Martime Mha. Hudhaifa Hajj aliahidi kutekeleza Mradi kwa wakati na kwa kuzingatia ubora.

Mradi wa uboreshaji huduma ya majisafi na usafi wa mazingira Morogoro unafadhiliwa na Serikali kupitia mkopo wenye masharti mafuu kutoka Shirika la maendeleo Ufaransa ba utagharimu zaidi ya Tsh. Bilioni 185 za kitanzania.



## KAMATI YA SIASA WILAYA YAPONGEZA KASI YA ULAZAJI BOMBA MRADI WA KIHONDA

Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Morogoro ikiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo Bw. Fikiri Juma iliipongeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) kwa kasi ya shughuli ya ulazaji bomba inayoendelea katika maeneo mbalimbali ikiwemo Kambi tano na nguvu tano katika utekelezaji wa Mradi wa Maji.

Pongezi hizo zilitolewa Oktoba 12, 2023 wakati Kamati hiyo ilipotembekea Ofisi za MORUWASA-Makao Makuu ikiwa sehemu ya ziara ya Kamati hiyo ya kukagua Miradi ya mbalimbali ya Maendeleo katika Wilaya ya Morogoro.

Pamoja na pongezi hizo Bw. Fikiri alitoa maelekezo kwa Taasisi za Umma kushirikiana ili kunapotokea mapungufu wakati wa utekelezaji wa Miradi ziweze kurekebishwa kwa wakati na wananchi waendelee kupata huduma.

Sambamba na hilo alieleza uwepo wa changamoto ya Upotevu wa Maji na kusisitiza ushirikiano baina ya TARURA na MORUWASA katika kukabiliana na upotevu wa maji hasa wakati wa utekelezaji wa Miradi ya barabara.

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa MORUWASA Mha. Tamim Katakweba akiwasilisha taarifa kwa ya utekelezaji wa Miradi mbalimbali itakayotatua changamoto ya maji katika Manispaa ya Morogoro na kubainisha Miradi ya Kasanga na Bigwa ambayo imekwishakamilika huku ikiendelea kunufaisha wananchi.

Mha. Katakweba aliongeza kuwa Mradi wa maji katika kata za Kihonda, Lukobe na Mkundi unaendelea kwa kasi na upo katika hatua nzuri ya utekelezaji huku upande wa Mradi Mkubwa wa Kuboresha Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro ukiendelea vizuri ambapo kukamilika kwa Miradi yote hiyo kwa pamoja utapelekea huduma ya maji katika Manispaa ya Morogoro kupatikana kwa zaidi ya asilimia 100 ifikapo mwaka 2025.



# TIB, MORUWASA KUIMARISHA USHIRIKIANO KATIKA UTATUZI WA CHANGAMOTO ZA MAJI MOROGORO

Bodi ya Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB) ilifanya ziara ya kikazi ya kutembelea Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) kwa lengo la kuimarisha ushirikiano katika juhudi za kuboresha upatikanaji wa huduma za Maji Morogoro.

Ziara hiyo ilihusisha kutembelea Mradi wa Tanki la Mguru wa Ndege ikiwa ni sehemu ya Mradi wa Uboreshaji Huduma ya Majisafi maeneo Kihonda, Lukobe, Kiegea, Mkundi, SGR na Viwandani.

Akiongea wakati wa ziara hiyo Mkurugenzi Mtendaji wa MORUWASA,Mha. Tamim Katakweba aliieleza bodi hiyo kuwa pamoja na kazi zingine za utekelezaji wa mradi zinazoendelea kwa sasa MORUWASA ipo katika mchakato wa kuhakikisha kunakuwa na nguvu kubwa katika kutekeleza maunganisho ya Maji ikiwa ni kutekeleza maelekezo ya Serikali ya kuhakikisha wananchi wa maeneo hayo wanapata huduma ya Maji kabla ya Disemba 25,2023.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya Uwekezaji Tanzania ,Bw. Sosthenes Kewe aliipongeza MORUWASA kwa mipango na kazi kubwa inayoendelea kufanya ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa Miradi ya Maji na kubainisha kuwa wao kama wadau wa maendeleo wapo tayari kushirikiana na MORUWASA katika kuwezesha utatuzi wa changamoto za Maji katika maeneo inayoyahudumia.

Awali Benki ya Uwekezaji Tanzania iliwezesha utekelezaji wa Mradi wa Maji safi wa Bigwa-Bohmela unaondelea kunufaisha zaidi ya wananchi 35,000 kwa kutoa Mkopo wa masharti nafuu wa takribani Tsh. Bilioni 2.4.

# MORUWASA YASHIRIKISHA WADAU MAPENDEKEZO YA BEI MPYA ZA MAJI

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) ilikutana na wadau mbalimbali na kupokea maoni yao kuhusu mapendekezo ya bei Mpya za huduma za Maji kwenye kikao kilichofanyika leo Agosti 24,2023 katika ukumbi wa Hoteli ya Edema, Morogoro.

Wadau mbalimbali kutoka maeneo yanayohudumiwa na MORUWASA ya Manispaa ya Morogoro, Miji ya Kilosa na Mikumi na maeneo ya Mkambarani, Dakawa, Dumila na Mzumbe waliweza kuwasilisha maoni yao kuhusu mapendekezo ya Bei Mpya yaliyowasilishwa na MORUWASA.

Awali akifungua kikao hicho, Mkuu wa Wilaya ya Morogoro Mjini Mhe. Rebeca Nsemwa aliipongeza MORUWASA kwa hatua ya kushirikisha wadau na kuwataka wajumbe hao kuzingatia maslahi mapana ya wananchi katika maoni yao.

Wadau mbalimbali walioshiriki kikao hicho ni pamoja na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Ofisi ya Mkurugenzi Manispaa ya Morogoro na viongozi wa Wilaya za Morogoro Mjini, Morogoro DC , Mvomero na Kilosa.

Wengine ni Viongozi wa Dini Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi na vyama vya upinzani, Waandishi wa Habari , Taasisi za Umma na wawakilishi wa wananchi Viwanda, Vyuo, Hoteli na wawakilishi wa mwananchi mmoja mmoja.

Maoni yaliyotolewa na wadau yatazingatiwa katika uboreshaji wa huduma na yatawasilishwa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ikiwa ni sehemu ya mchakato wa kuidhinisha bei mpya za huduma za maji zitakazotumika mpaka 2025/2026.



# MORUWASA YARUDISHA KWA JAMII YA WATOTO YATIMA

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) ilitembelea kituo cha RAYA ISLAMIC ORPHANAGE CENTRE, makao ya kulelea watoto yatima na waishio katika mazingira magumu kilichopo Lugono na kukabidhi msaada wa mahitaji mbalimbali.



Akizungumza mara baada ya kupokea msaada huo,muanzilishi na msimamizi wa kituo hicho Bi. Raya Subaha aliishukuru na kuipongeza MORUWASA kwa kuguswa na kufika kituoni hapo.

Aidha Bi. Raya alisema kituo kina changamoto mbalimbali na uhitaji wa misaada hivyo ameomba taasisi na jamii kwa ujumla kuguswa na kuwasaidia mahitaji mbalimbali kwani watoto hao ni wetu wote.

Naye Kaimu Mkuu wa kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma MORUWASA Bi. Neema Nyangi alisema kuwa MORUWASA imetoa msaada huo ikiwa ni sehemu ya utaratibu wa Mamlaka wa kurudisha kwa jamii katika nyanja mbalimbali.

Pia alitoa wito kwa jamii na Taasisi zingine na mtu mmoja mmoja kuguswa na kutoa misaada kwa jamii zenye uhitaji maalum ili kuwawezesha kupata mahitaji ya kimsingi na kuwasaidia kutimiza ndoto zao kama watoto wengine.

# PROGRAMU YA WATERWOX KUSAIDIA KUNUSURU VYANZO VYA MAJI MOROGORO

Shirika la World Waternet kupitia programu ya WaterWox kwa kushirikiana na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Morogoro (MORUWASA) pamoja na Bodi ya maji Bonde la Wami/Ruvu iliendesha warsha ya siku tatu ya kujadili namna ya kuanzisha kilimo msitu katika kidakio cha Bwawa la Mindu.



Aidha, warsha hiyo ililenga kurejesha uoto wa asili katika safu za milima ya Uluguru pamoja na kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji vinavyotiririsha maji yake kwenye Bwawa la Mindu pamoja na kuanzisha kilimo cha mazao rafiki kwa maji chenye faida za kiuchumi kwa jamii inayoishi pembezoni mwa vyanzo vya maji.

Warsha hiyo ilianza Agosti 29,2023 katika ukumbi wa 'Maji House' uliopo jengo la makao makuu ya ofisi ya . Bodi ya Maji ya Bonde la Wami/Ruvu mkoani Morogoro pia imehudhuriwa na Taasisi mbalimbali ikiwemo TAFORI, Agro Wezesha na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) ambao ni wadau muhimu wa kuhifadhi mazingira



# MHE. JAFO AIPA HEKO MORUWASA

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Dkt. Selemani Jafo aliipongeza jitihada zinazofanywa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) katika kuhakikisha inamtua mama ndoo kichwani.

Mhe. Jafo, alitoa pongezi hizo leo Agosti 7,2023 alipotembelea Banda la MORUWASA kwenye maonesho ya Nanenane kanda ya Mashariki yanayoendelea katika viwanja vya J.K. Nyerere mkoani Morogoro.

Aidha, aliitaka MORUWASA kuendelea kutoa elimu ya utunzaji wa mazingira ikiwa ni pamoja na elimu ya kuzuia shughuli za kibinadamu zinazofanyika pembezoni mwa vyanzo vya maji ili kuepusha kujaa kwa tope katika Bwawa la mindu ambalo ni chanzo mama cha maji kwa wakazi wa Morogoro.

Sambamba na hilo alisisitiza juu ya utoaji wa elimu kuhusu athari ya vitendo vya uchomaji moto wa misitu iliyopo katika Milima ya Uluguru ili kuhifadhi mazingira na vyanzo maji.

MORUWASA ilishiriki maonesho ya nanenane huku ikisogeza karibu huduma mbalimbali zinazotolewa na Mamlaka hiyo pamoja na utoaji wa elimu ya umuhimu wa utunzaji wa Mazingira na vyanzo vya maji kwa wananchi wanaojitokeza katika

# MORUWASA YASAINI MKATABA NA EGIS WATER AND MARITIME JV ICE PROJECT SERVICES LTD

Kufuatia maagizo ya Mh. Nadhifa Kemikimba, Katibu Mkuu Wizara ya Maji wakati wa ziara yake ya kikazi ya Juni 22,2023 mkoani Morogoro, yaliyoitaka Menejimenti ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) kuongeza kasi ya kutekeleza ujenzi wa Mradi mkubwa wa kuboresha Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro wenye thamani ya Tsh Bilioni 185.

Julai 21,2023 MORUWASA ilisaini Mkataba na Mtaalamu Mshauri, Kampuni ya Egis Water and Maritime ya Ufaransa inayoshirikiana na ICE Project Service Ltd ya Tanzania, ambaye atatekeleza kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Usanifu wa kazi za ujenzi wa miundombinu ya maji, Utayarishaji wa nyaraka za zabuni za kupata Wakandarasi, Kuandaa Mpango Mkuu wa usambazaji maji 'Water Supply Master Plan', pamoja na usimamizi wa kazi zote za ujenzi katika Mradi ikiwemo kunyanyua Bwawa la Mindu na kujenga mtambo mpya wa kutibu maji 'Mafiga' wenye uwezo wa kuzalisha lita Milioni 54 kwa siku.

Akiongea wakati wa zoezi hilo Mkurugenzi Mtendaji wa MORUWASA Mha. Tamim Katakweba aliwapongeza Egis Water &Maritime na ICE Project Service Ltd kwa kushinda zabuni hiyo na kuwaahidi kuwapa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yao.

Aidha, Mha. katakweba alisisitiza kuwa usanifu lazima uguse maeneo yote ikiwemo Lugala, Lukobe, Mkundi, Kihonda, Mkundi, Makunganya, Magorofani, Nane Nane, Tungi, Tubuyu, Kingolwira, Kitungwa, Kipera, Kola, Knyembe na Mjini Kati.

Pia Mha.Katakweba aliisisitiza kutekeleza kazi kwa ufanisi mkubwa na kuhakikisha mradi unakuwa na ubora na viwango vya hali ya juu.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa ICE Project Service Ltd Mha.Andrew Mwakagenda aliishukuru MORUWASA na kuahidi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuhakikisha wananchi wa Morogoro wanaanza kunufaika na Mradi ifikapo 2025.



# KM WIZARA YA MAJI AITAKA MORUWASA KUONGEZA KASI UTEKELEZAJI MRADI MKUBWA WA MAJI MOROGORO

Katibu Mkuu Wizara ya Maji Mhandisi Nadhifa Kemikimba aliiagiza Menejimenti ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) kuhakikisha inaongeza kasi katika utekelezaji wa Mradi Mkubwa wa Uboreshaji Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Manispaa ya Morogoro.



Mhandisi Kemikimba aliyasema hayo wakati wa ziara yake ya kutembelea Taasisi za Sekta ya Maji Morogoro ambapo pamoja na mambo mengine alikutana na Menejimenti ya katika Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) na kufanya tathmini ya maendeleo ya utekelezaji wa Mradi huo unaofadhiliwa na Serikali kupitia mkopo wenye masharti nafuu kutoka Shirika la Maendeleo la Ufaransa ( AFD) kwa thamani ya shilingi Bilioni 185.

Mha. Kemikimba aliielekeza Menejimenti ya MORUWASA na timu inayotekeleza mradi huo kufanya marejeo ya muda wa utekelezaji wa vipengele vya mradi ikiwemo Unyanyuaji wa Bwawa la Mindu, Ujenzi wa Mtambo Mpya wakutibu Maji Mafiga uwezo wa kuzalisha maji lita 54,000,000 kwa siku na ujenzi wa Ofisi Mpya za Mamlaka ili kuongeza kazi ya utekelezaji na kuhakikisha mradi unakamilika mapema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa MORUWASA Mha. Tamim Katakweba alipokea maagizo ya Katibu Mkuu na kuahidi kuyatekeleza.

Katika hatua nyingine ya ziara hiyo Mhandisi Kemikimba alikutana na watumishi wa MORUWASA na kuwapongeza kwa kazi kubwa na jitihada wanazozifanya katika kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maji pamoja na kuendelea kutoa huduma ya maji kwa wananchi.

Aidha, aliwasisitiza watumishi wa MORUWASA kuwa pamoja na jitihada kubwa wanazozifanya bado wana kazi kubwa ya kufanya na kuwa mafanikio ya miradi ya maji na Taasisi ni jukumu la watumishi wote na kuwataka kuendelea kufanya kazi kwa moyo mkunjufu.

"Muendelee kufanya kazi kwa moyo mkunjufu muipende kazi yenu, muipende Taasisi yenu,muwapende viongozi wenu" alisisitiza Mhe. Kemikimba.

Ziara hiyo ya Katibu Mkuu Wizara ya Maji ilihusisha Taasisi za Sekta ya Maji Morogoro ikiwemo Bodi ya Maji Bonde la Wami Ruvu, RUWASA mkoa wa Morogoro na Maabara ya Ubora wa Maji Morogoro.




# MHESHIMIWA MWASA AZINDUA RASMI KAMPENI YA UPANDAJI MITI MOROGORO

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Mhe. Fatma Mwasa alizindua rasmi kampeni ya upandaji miti katika mkoa wa Morogoro yenye lengo la kurejesha uoto wa asili na kulinda na kuhifadhi mazingira pamoja na vyanzo vya maji.

Uzinduzi huo ulifanyika Aprili 21,2023 kando ya Bwawa la Mindu ambapo aliweza kuongoza viongozi na wadau wengine wa Mazingira katika mkoa wa Morogoro ikiwemo MORUWASA katika shughuli ya kupanda miti rafiki na maji.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo Mhe.Mwasa aliwataka wananchi kuliheshimu Bwawa la Mindu ili liweze kusaidia wananchi wa Morogoro kwa miaka mia moja ijayo.

"Bwawa la Mindu ni chanzo kikuu cha Maji kwa wakazi wa Mkoa wa Morogoro tunatakiwa kuliheshimu na kulienzi ili liweze kutuendeleza kwa miaka hamsini hadi mia moja ijayo"

"Serikali imetenga Tsh bilioni 185 kwa ajili ya kulipanua Bwawa hilo na tayari tenda zimeshatangazwa"

Sambamba na hilo Mhe. Mwasa alisistiza kuwa Bwawa la Mindu linalindwa na kikosi maalum cha jeshi na amewaasa wananchi kuacha kuchoma miti hovyo kwani kwa wale watakaofanya hivyo watachukuliwa hatua kali za kisheria.

"Kuna wale wanaochoma moto niwatangazie rasmi Bwawa hili linalindwa na kikosi maalum cha jeshi lakini pia wakisaidiana na askari wa jeshi la akiba

"Ukiunguza ukichoma miti hovyo jela miaka saba, Jela miaka saba bila utani kwa mujibu wa sheria" Amesema

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Bodi ya Maji, Bonde la Wami/ Mhandisi Elibariki Mmasy aliahidi kuwa eneo hili lililozunduliwa na Mhe. Mwasa litafanywa kuwa la mfano kwa mkoa wa Morogoro.



# BODI ZA MORUWASA NA WAMIRUVU ZAKUTANA KUNUSURU VYANZO VYA MAJI MOROGORO

Bodi za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) na Bonde la Wami/Ruvu (WRBWB) walikutana kwa lengo la kujadili kwa pamoja hali ya rasilimali ya Maji kwa lengo la kuwa na mikakati ya pamoja ya kunusuru vyanzo vya maji na kuvifanya kuwa endelevu ili kuhakikisha huduma ya Maji iliyo toshelevu na ya uhakika inapatikana kwa wananchi wa Morogoro.

kikao hicho kilifanyika Aprili 5,2023 katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa MORUWASA na kufuatiwa na ziara ya kutembelea Bwawa la Mindu na baadhi ya mito inayotiririsha maji katika Bwawa hilo, ambapo wajumbe wa Menejimenti za MORUWASA na Bonde la Wami/Ruvu wameweza kushiriki.

Pamoja na Bodi ya Wami/Ruvu kuainisha mikakati katika kulinda Vyanzo vya Maji na Mabanio ikiwa ni pamoja na kuweka uzio na bikoni katika maeneo hayo,Pande zote mbili ziliazimia kuongeza ushirikiano katika kuhakikisha vyanzo vya maji vilivyopo vinatunzwa na kuendelezwa, kuhakikisha kunakuwa na ushirikishwaji wa Mamlaka zingine kama halmashauri na ofisi ya Mkuu wa Mkoa,Wadau na Wananchi kwa ujumla katika kutekeleza mikakati mbalimbali ya kulinda na kuendeleza rasilimali ya maji.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya MORUWASA Prof. Romanus Ishengoma alisema pande zote mbili hazina budi kuendelea kuimarisha mahusiano katika kutekeleza azma hii kwani wote ni

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Bonde la Wami/Ruvu Bi. Hafsa Mtasiwa alisisitiza kuwa Bonde la Wami/Ruvu na MORUWASA zote ni Taasisi ambazo ndugu na zinategemeana kwa kiwango kikubwa katika kuhakikisha wananchi wa Morogoro wanapata huduma muhimu ya maji na kuongeza kuwa suala la utunzaji na uendelezaji wa vyanzo vya maji lisiachwe kwa Bonde la Wami/Ruvu pekee kwani ni

# BODI YA MORUWASA YAZUNGUMZA NA WATUMISHI

"Niseme madhumuni ya kikao hiki ni Mwenyekiti wa Bodi kutoa fursa kwa wafanyakazi kusema" hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa Bodi ya MORUWASA, Prof. Ishengoma wakati akifungua kikao cha Bodi ya Wakurugenzi na Watumishi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) kilichofanyika Aprili 6,2023 katika hoteli ya Nashera.



Pamoja na mambo mengine watumishi wa MORUWASA waliweza kutumia fursa hiyo kuwasilisha maoni yao mbalimbali kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kiutendaji na kuboresha utoaji huduma kwa wateja na wananchi wanaohudumiwa na Mamlaka hiyo.

Akiongea wakati wa kupokea maoni kikao Mwenyekiti wa Bodi ya MORUWASA, Prof. Romanus Ishengoma aliwapongeza watumishi kwa maoni mazuri waliyowasilisha na kwamba maoni hayo yamepokelewa na yatafanyiwa kazi na Menejimenti ya MORUWASA.

Aidha kikao hicho kilitanguliwa na kikao cha Baraza la watumishi ambapo watumishi waliweza kuchagua viongozi wa Baraza la Wafanyakazi wa pamoja na kuchagua viongozi wa SACCOS ya Mamlaka hiyo.

"Niwapongeze, wale waliochaguliwa ni dhamana kuwawakilisha wenzenu" alisema Prof. Ishengoma

# EWURA CCC YAPONGEZA MIKAKATI YA MORUWASA

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji ( EWURA CCC) limepongeza jitihada na mikakati iliyowekwa na MORUWASA ya kuhakikisha changamoto ya maji Morogoro inamalizika.

Pongezi hizo zilitolewa Juni 8,23 na Kaimu Katibu Mtendaji wa EWURA CCC Bi. Stella Lupimo wakati wa ziara ya Bodi na Wajumbe wa baraza hilo ya kutembelea na kujifunza shughuli zinazotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA).

Bi. Stella alisema wamejionea namna MORUWASA ilivyojipanga katika kutatua changamoto ya maji Morogoro.

Naye, Mkurugenzi Mtendaji wa MORUWASA Mha. Tamim Katakweba akiwasilisha taarifa ya hali ya upatikanaji wa maji kwa maeneo yanayohudumiwa na MORUWASA pamoja na mikakati inayotekelezwa na MORUWASA alisema kukamilika kwa miradi mbalimbali ya muda mfupi na kati inayoendelea kutekelezwa itapelekea Manispaa ya Morogoro kuwa na uhakika wa huduma ya maji kwa zaidi ya asilimia 100.

# "SITAKUWA NA MZAHA KATIKA SUALA LA UTUNZAJI WA VYANZO VYA MAJI"

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro Mhe. Rebeca Nsemwa alisema kuwa hatokuwa na mzaha katika suala la utunzaji wa vyanzo vya maji.

Mhe. Nsemwa aliyasema hayo wakati wa akifungua bonanza la michezo ikiwa ni moja shughuli ya kilele cha maadhimisho ya wiki ya maji iliyofanyika Machi 22,2023 katika uwanja wa Tumbaku,Morogoro Mjini.

Aidha Mhe. Mkuu wa Wilaya aliipongeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi Mazingira Morogoro na Bodi ya Maji, Bonde la Wami/Ruvu kwa Ubunifu wao kutumia Bonanza la Michezo kwa lengo la kuhamasisha na kusambaza ujumbe kuhusu masuala ya Maji.

Kabla ya uzinduzi wa Bonanza hilo lililoandaliwa na MORUWASA kwa kushirikiana na Bodi ya Maji,Bonde la Wami/Ruvu Mhe. Nsemwa alifanya ziara ya kutembelea Kidakio cha Mambogo na Mtambo wa kusafisha maji wa Mambogo.

Kwa upande wake Mkurungenzi Mtendaji wa MORUWASA Mhandisi. Tamim Katakweba alizungumzia mikakati ya MORUWASA katika kuhakikisha wanafikia kiwango kubwa cha kuzalisha huduma ya maji na kuwasambazia wananchi kwa kuainisha miradi mbalimbali iliyotekelezwa na inayoendelea kutekelezwa na Mamlaka hiyo.

Maadhimisho ya wiki ya maji ambayo hufanyika tarehe 16-22 Machi kwa mwaka huu wa 2023 yalibeba kauli mbiu "Kuongeza Kasi katika Sekta ya Maji kwa Maendeleo Endelevu ya Uchumi" Ambapo MORUWASA iliweza kutekeleza maadhimisho hayo kwa kujikita zaidi katika kuelimisha na kuhamasisha Umma kuhusu Huduma na Mikakati ya MORUWASA.



# HABARI PICHA



Picha za tukio la Uzinduzi wa mradi wa Uboreshaji wa Huduma ya Maji Kauzeni uliozinduliwa tarehe 13 Mei, 2023 na Mwenge wa Uhuru uliongozwa na ndugu Abdalla Shaib Kaim.











# HABARI PICHA



Picha za ziara  Ujumbe wa Wizara ya Maji kutathimini maendeleo ya miradi ya maji inayotekelezwa na MORUWASA iliyofanyika tarehe 7 Juni, 2023 ambapo walitembelea Mradi wa uboreshaji huduma ya maji Kihonda, Kiegea, Mkundi, Lukobe na SGR Nna Mradi wa Uboreshaji huduma ya majisafi na majitaka Manispaa ya Morogoro wenye thamani ya Tsh. Bilioni 185.









MORUWASA

WASILIANA NASI NA FUATILIA KURASA ZETU ZA MITANDAO YA KIJAMII ILI KUPATA TAARIFA ZAIDI

0800751011 **(BURE)**

0736 737 736

@moruwasa

@moruwasa2

Moruwasa Digital

www.moruwasa.go.tz